
# UMEBADILIKA

HADITHI FUPI



MWANAWETU MMUNI

# YALIYOMO

DIBAJI ........ 3

UTANGULIZI ........ 5

MWANTUM NI NANI? ........ 6

HOSPITALINI ........ 16

MKE MDOGO WA LEMU ........ 18

USHAURI WA MJOMBA ........ 27

# DIBAJI

Kuna baadhi ya wanawake na wanaume wanatafsiri vibaya malengo ya Mkutano Mkuu wa Wanawake uliofanyika mjini Beijing, nchini China mwaka 1995. Watu wanajiuliza, “hivi Mkutano wa Beijing uliwafundisha wanawake kutesa au kunyanyasa familia zao hasa wanaume (mume)?” Jibu ni HAPANA.

©2021

Haki Miliki @ Mwanawetu Mmuni

Mwanawetu Mmuni

P. O Box 90,

Mtwara

**TANZANIA**

Simu: +255 737966996

©2021

# UTANGULIZI

Simulizi hii inahusu wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia ulioegemea kwenye uhusiano wa kimapenzi. Mhusika mmoja ni msichana msomi aitwaye Mwantum aliyejipatia elimu yake ya juu, nje ya nchi. Wakati anakwenda masomoni, Mwantum aliahidiana na Ahmad kuwa watafunga ndoa pindi atakapomaliza masomo yake na kurejea nchini Tanzania. Lakini mambo yalikwenda ndivyo sivyo baada ya Mwantum kuhitimu elimu ya Chuo Kikuu.

Mzee Lemu ana Wake watatu. Miongoni mwao, yumo mwanamke aliyehisiwa kuwa sio mwaminifu na kusababisha hofu yakupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa ukiwemo UKIMWI.

Pia ndani ya hadithi hii, Malisara aliamua kumuacha mkewe na kutafuta mwanamke wa nje (mchepuko).

## MWANTUM NI NANI?

Mwantum Shemzima ni binti mrembo, aliyepata elimu yake ya juu katika chuo cha Udaktari nchini India. Akiwa anaendelea na masomo huko ughaibuni; Mwantum alianzisha uhusiano wa kimapenzi na Mwanachuo mwenzie kijana mmoja kutoka Mombasa Kenya aitwaye Kamau. Wawili hao walishiriki chuo kimoja ijapokuwa Kamau alisomea kozi ya Famasia.

Baada ya kuhitimu elimu yao ya juu, wote wawili walirejea nyumbani ili kuyatumikia mataifa yao kama soko la ajira lilivyohitaji. Walianza kuwasili nchini Tanzania kabla ya Mombasa Kenya ili kuanza kufanya taratibu za kukamilisha uhusiano wao kwa kutambulishana kwenye familia. Ujirani wa miji ya Tanga na Mombasa ndiyo uliotoa fursa ya kuwaweka vijana hawa karibu hadi kuwa wapenzi. Khaa! Undugu wa ugenini!

***

Katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, kulikuwepo kijana mmoja anayehangaika, na kukosa utulivu kabisa! Alitembea huku na huko, akiwa amebeba maua na mfuko wa fasheni uliotengenezwa kwa malighafi za plastiki.



Ulisheheni bidhaa ambazo hazikuweza kujulikana lakini ilionesha kuwa ni muhimu sana kwa kijana huyo kwasababu alikuwa anafungua mfuko huo na kuchungulia kuona vilivyomo ndani mara kwa mara. Pia alikuwa akigeza namna ya kukumbatia mtu,

akicheka na kufurahi peke yake. Watu waliokaribu nae walistaajabu na kujiuliza maswali;

“Kwani kijana huyu, anapiga picha za sinema?” Kwa kuwa hakuwepo wakutoa majibu, waliendelea kushuhudia vimbwanga hivyo hadi pale iliposikika sauti ya tangazo lililoeleza kuwasili kwa ndege ya Qatar kutoka Doha. Geti lilifunguliwa na watu wote waliingia akiwemo kijana huyo barubaru.

***

“Mwantum! Mwantum!”

“Nani ananiita?” alijiuliza Mwantum na kugeuka kuangalia upande uliotoka sauti hiyo. Alikutana na sura ya kijana iliyotawala tabasamu pana.

“Ooh! Mpenzi! Laazizi wangu! Mwandani wangu! Umerudi? Karibu Tanzania, karibu nyumbani. Asante Mungu kwa kukurejesha salama.” Alimfuata

Mwantum na alipomfikia, alimkumbatia na kuomba busu.

Haukuwepo kushuhudia masaibu hayo lakini yaweza kuwa malaika wako walikuwepo! Kilichomkuta kijana huyo mtanashati na mchangamfu kupitiliza, kilimfanya agande damu kama samaki frijini au picha ya mnato kutokana na mapokeo ya mrembo aliyemwita "Laazizi" usiojali kaumu. Kweli dunia hadaa, ulimwengu shujaa.

"Usinishike!" Mwantum alijibu kwa hasira na kumsukuma kijana huyo.

"Mwantum, mpenzi wangu! Naomba usinifanyie hivyo, unajua jinsi gani ninavyokupenda. Mimi ni yule yule mumeo mtarajiwa, Ahmad, na kumbuka ahadi yetu hakika muda umeshatimia. Tafadhali ninakuomba ukubali kupokea zawadi niliyokuandalia na tukafanye sherehe.

“Nyamaza kimya! Halafu kijana koma, mimi sio mpenzi wako na wala sifanani kuwa mpenzi wako. Unamuona huyu?” alimuoneshea kidole Kamau aliyesimama pembeni yake.

Maneno makali aliyotumia Mwantum kumuonya Ahmad ili aache akua na kumsonga, yalimsononesha na kumfanya kupata fadhaa. Jakamoyo liliendelea baada ya Mwantum kutoishia kuongea pekee bali alimsukuma kando kwa nguvu. Ahmad alidondoka chini na kupoteza fahamu, maua na mfuko vilisambaratika.



Mashuhuda wa tukio hilo walisogea karibu ili waweze kujua kinachoendelea.

“Kulikoni unamkana mwenzio kama humjui? Kwa haraka haraka inaonesha mnajuana. Ona sasa ulichokifanya! Wanawake…..!” Aliongea kijana mmoja aliyesogea na kuchuchumaa karibu na Ahmad na kuanza kumpepea kwa kutumia kipeperushi alichoshika mkononi.



Kuona hivyo Mwantum aliingia garini akifuatwa na Kamau.

“Tuondoke!” Dereva Taxi  aliondoa gari haraka baada tu ya geti kufunguliwa.

***

Ndani ya gari;

“Mpenzi, yule kijana ni nani?” Kamau alimuuliza Mwantum bila kumwangalia usoni, akiwa ameikunja sura kwa hasira.

“Ni jirani yetu. Unajua utoto! Unaweza ukawa na ahadi zisizotimizika. Utotoni tuliwahi kupanga kufunga ndoa na kuishi pamoja kama mke na mume baada ya kuhitimu masomo. Hivyo ninahisi mwenzangu bado anayo na kushindwa kujiongeza kwa kusoma alama za nyakati akashika zake nami nishike zangu. Hilo ndilo lililonigharimu leo, Wahenga husema; ‘ukicheka na mbwa, utaingia nae msikitini.” Alijitetea, akijidekeza akiwa anachua mapaja ya Kamau kwa kutumia mikono

yake laini yenye kubeba kucha ndefu mithili ya vidole vya mwewe.

“Hivyo tu? Unadhani mimi ni mjinga? Yule ni mwanaume kama mimi, unasikia?”

“Samahani mahabubu. Naomba uvute subra, tutazungumza tukishafika tuendako. Amini, nakupenda sana mpenzi wangu!” alisema Mwantum kwa sauti nyororo iliyotokea puani. Sauti hii ilikuwa kama ugoro wa Kimasai kwenye fikra za Kamau.

“Sawa! Lakini nimeamua kufikia hotelini badala ya nyumbani kwenu kama tulivyopanga.” Alijibu Kamau akiwa anaonesha kutoridhika na majibu aliyopewa na mpenzi wake, yaliyomfanya awe na msongo wa mawazo.

“Unakumbuka tumeandaliwa tafrija? Sio vizuri kuwasusia wazee shughuli waliyoiandaa kwa ajili ya vijana wao vipenzi. Aula wangu, naomba twende

kwanza nyumbani halafu baadae tutakwenda hotelini kupumzika. Sawa mpenzi?" Alimbusu shavuni kwa mahaba.

"Tafrija? Kwa hali hii ya majirani kuja kutangaza harusi mapokezi! Mwenye sherehe yake tumemwacha uwanja wa ndege. Mimi mgeni mwalikwa hata kama nikikosa kuhudhuria hakuna ubaya. Ninatakiwa nijipe muda wa kutafakari kwa kina yasije yakanikuta ya jirani yako."

Mwantum alipata hofu na kujiona yupo njia panda, tena kwenye mataa yasiyobadilika rangi. Lakini alijikaza nakujibaraguza kama hakuelewa alichomaanisha Kamau. Alisema;

"Sawa ninakubali tukafikie hotelini kisha tutafikiria siku ya kwenda nyumbani. Nitamjuza Baba afanye mabadiliko ya siku ya sherehe kabla ya watu kuingia

ukumbini.” Alishusha pumzi kama mtu aliyetua Mzigo.

Kamau alimwangalia Mwantum bila kutoa neno. Akiwaza, “akili kichwani mwangu. Mimi ni mtoto wa Mombasa! Najua tofauti ya tetere na njiwa. Utafurahi mwenyewe!” Alitabasamu.

Mwatum alipoliona tabasamu la Kamau, alipata matumaini ya kuwa pendo lake bado alijafukaa. Moshi unaofuka ulidhihirisha uwepo wa moto. Kumbe moyo ni kichaka, hivyo watu wema na waovu hujificha. Mwantum alimuegemea Kamau, nae bila hiana alimpokea na safari ya kwenda hotelini iliendelea.

# HOSPITALINI




Ahmad alifumbua macho na kujikuta yupo juu ya kitanda hospitalini, alikopelekwa kwa msaada wa wasamalia wema. Pembeni ya kitanda aliketi mjomba wake, Mzee Lemu.

“Alhamdulillah!” aliinua mikono juu kutoa shukrani. ‘Vipi, unaendeleaje?" aliuliza Mzee Lemu.

“Sijambo!” alijibu Ahmad.

“Una uhakika?”

“Nipo vizuri.” Alijaribu kuinuka ili akae kitako lakini alishindwa ndipo Mjomba wake alipomsaidia.

“Unakumbuka kilichokutokea?” Mzee Lemu alimuuliza Mpwa wake. Alitoa tabasamu kumchangamsha kwa utani.

Ahmad alitabasamu pia bila kutamka chochote, badala yake alidondosha matone ya machozi mashavuni.

“Unafanya nini sasa? Umenijibu, hakuna tatizo. Machozi yanatoke’aje? Jikaze usilie. Wanaume hawalii. Ni aibu kwa familia kuwa na mwanaume anayelia, hasa kulizwa na mwanamke. Acha kulia na futa machozi haraka! Watakukuta watu.” Ahmad alifanya kama alivyoelekezwa.

Ilisikika sauti ya hatua za mtu aliyeelekea chumbani humo, na ghafla mlango ulifunguliwa. Alikuwa Nesi aliyefika kuendelea kutoa matibabu.

# MKE MDOGO WA LEMU

Baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali, Ahmad akiwa mwenye afya tele, alikwenda moja kwa moja nyumbani kwa Mzee Lemu kabla ya kupita nyumbani kwake;

“Hauna haja ya kunisimulia kilichotokea. Tayari nilishasimuliwa na mashuhuda. Pole sana  Mpwa’ngu, hao ndiyo wanawake wa zama hizi waliobarikiwa upendo zaidi ya mama zetu na ukatili zaidi ya jambazi. Wanatumia fomula kupenda, sasa chemsha bongo kuhakikisha mambo yanakwenda sawa. Kosa moja, goli moja! Ukiona umeelemewa, usimtafute mchawi bali ujue kuna mahali umekosea kucheza. Unamkumbuka shangazi yako, Mke wangu mdogo niliyeletewa na Nyanya yako toka kijijini?” Mzee Lemu alimkumbusha Ahmad.

“Ninamkumbuka. Shangazi Aisha! Niambie, kuna shida gani?” aliuliza kwa kudadisi.

“Aisha alikuwa mke niliyemridhika kwa kukidhi hitaji la mwili wangu, kuliko wake wengine wote kwa kuwa alikuwa mtaalamu kitandani. Ni fundi kweli kweli, pia alikuwa msafi, na mpishi nzuri wa vyakula mbalimbali. Nilijitoa kafala kwa kumtimizia mahitaji yake au kufanya kila alichokitaka ili kuhakikisha ninaendelea kula raha kwa kufurahia penzi lake. Sikupitisha siku bila kwenda nyumbani kwake ingawa niliweka zamu za siku tatu tatu za kulala kwa kila mke. Lakini nilipita kwa Aisha kwanza kabla ya kwenda kwengineko. Ubaya gani nilikuwa ninawafanyia wake wengine?” alinyamaza kupisha mate yalainishe koo kisha kuendelea na mazungumzo yenye simulizi ya misukosuko ya jahazi la maisha na mapenzi.

“Kwa bahati mbaya aligundua siri yangu, akaanza kuleta karaha na kwa kweli nilikosa raha kwasababu

nilikuwa sina chaguo la kukataa akitakacho hata kama kilikuwa kinagharama ya damu. Hakuishia kulazimisha visivyostahili pekee badala yake alianza kuacha nyumba shaghalabaghala, vyakula vibichi mezani ukiwa mgomo baridi ili nikale kwenye zamu, unyumba hadi siku ya zamu na mara kwa mara nilimkuta barazani kwenye maongezi na marafiki zake wakati ni kinyume na mila zetu kwa mwanamke kukakaa barazani kusogoa. Mwanamke sehemu yake yakukaa ni jikoni au ukumbini mlango ukiwa umefungwa. Pia mwanzoni mwa mapenzi yetu yaani nilipomuoa, alikuwa hodari wa kuacha akifanyacho hata kama ni misuko ya nywele na kunifuata ndani kunisikiliza lakini baada ya kupitiwa na chamchela, aliacha na kunisindikiza kwa macho sambamba na kicheko cha ngebe kama kuku mwenye mayai anapotoka nje.



Kuna wakati nilikutana na matukio yaliyonitikisa hadi nilijikuta mwili wangu ukiishiwa nguvu na ndipo nilipogundua mapenzi yanauma na waweza kufa kibudu. Mfano siku moja nilikutana uso kwa uso na kijana balehe akitoka ndani akifuatwa na Aisha, sasa angenidandanya ili nijifariji kuwa alikuwa ni ndugu yake! Alinijibu vibaya mbele ya kijana huyo mchanga, maneno yake yalikuwa kama chumvi kwenye kidonda kibichi. Aligoma kuniomba msamaha ingawa alikubali kuwa kijana niliyemuona ni mpenzi wake anayemfikisha kileleni. Sikutaka kuamini kuwa

pushapu zote ninazozipiga muda mwingine usiku wa manane au alfajiri mapema, niliambulia patupu hadi nilihitaji kifaranga kinipe msaada.”

‘Ingawa nilipitia kipindi kigumu chenye misukosuko ya mapenzi na uhusiamo kwa ujumla sababu, hadi wake wenzake wawili walikuwa wakilalamikia tabia yake. Nilijaribu kuomba suluhu ili Aisha abadilike na tuendelee na maisha yetu niliyoyapa jina la ‘u-ta-mu’ lakini sikufua dafu.” Mzee Lemu alikohoa kikohozi kikavu na kuendelea.

“Usiku mmoja, Mke mkubwa alighadhibika kuhusu mwenendo wa maisha yetu. Alisema kumekuwa hakuna tofauti na kusema; kuwa ninawalazimisha kuwafunga kafani wangali hai. Pale alipokumbusha juu ya uwepo wa maambukizi ya magonjwa ya zinaa yanayoambukizwa kwa kujamiina hasa Virusi vya UKIMWI. Aliniumiza na kinitafakarisha sana pale aliponiambia, endapo Aisha atapata maambukizi ya

magonjwa hayo na kushiriki nami tendo la ndoa bila kutumia kondomu ninakuwa kwenye hatari ya kuambukizwa pia. Alikadhirika nikifanya hivyo kwa Wake zangu wengine na wao nitawaingiza kwenye mtandao hatari wa maambukizi ya magonjwa hayo hatari. Niliogopa sana na ukizingatia mwanandoa kutumia mipira yao migumu ni karaha tupu. Ndio maana unapofikia umri wa kuoa, ni vema ukaoa ili kuepuka kutumia vitu vya bandia katika shughuli halali. Fikiria ni vigumu kulala na soksi miguuni, itakuwa mpira wakubana utupuni? Sasa, mimi ndiye niliyejitoa mhanga lakini itakuaje juu ya afya ya wanawake (wake) zangu wengine pamoja na watoto wao? Nilihisi harufu ya damu ikipenya puani mwangu, iliyotokana na misiba niliyoisababisha kutokana na tamaa yangu ya mwili."

Mke mkubwa alinitaka twende zahanati tukachunguzwe afya halafu baada ya hapo hatoshiriki

tendo la ndoa namimi hata kama sote tutakuwa hatujapata maambukizi, labda kwa kutumia kondomu. La sivyo, alitishia kudai talaka ili akaugulie nyumbani endapo itakuwa tayari ameshapata maambukizi. Alisema,”

“Ukiendelea kumwacha Aisha kwenye maisha yetu na kumtambua kama Mke wako, mimi ninakwenda nyumbani kwetu kijijini hata kama ukikataa kunipa talaka yangu. Kwasasabu utakuwa umeamua kutuua kutokana na ubinafsi wako. Kwa umri niliokuwa nao sitaweza kuvaa pampasi kama mtoto mchanga, niache nikafie nyumbani.”

“Alilia usiku kucha! Nilibembeleza hadi nikajikuta ninalia kwa hasira. Ilibaki kidogo nimnase vibao lakini nilijua, kilio chake kimetokana na matendo yangu. Na anachokifanya ni kutete uhai wake hivyo niliendelea kumrai anipe nafasi ya kufanya maamuzi magumu.”

“Kilifuata nini baada ya matukio hayo?” Ahmad aliuliza akiwa anakaa vizuri kama mtu aliyekurupushwa toka usingizini.

“Ilipofika asubuhi, nilikwenda kumwacha Aisha na kumrudisha kwa mzazi wake kijijini sababu alibakiwa na Mama pekee, Baba yake alishafariki. Aisha hakuonesha kujutia talaka badala yake alifurahia ingawa mama yake alilia na kusikitika sana. Alionesha kutofurahia tabia mbaya ya mtoto wake lakini haikusaidia kwakuwa nilimuoa Aisha na sio Mama Aisha. Huo ukawa mwisho wa Aisha katika maisha ya familia yangu lakini bado ninampenda sana siwezi kuudanganya moyo wangu kuacha kukumbuka raha na starehe niliyoipata toka kwake.” Mzee Lemu alimaliza kusimulia tukio hilo kwa huzuni akirudia kutaja jina la Aisha.

“Mmh, dunia haina huruma. Unaweza kumpenda mtu ambaye hana chembe ya hisia nawe.” Alisema Ahmad kwa masikitiko.

***

## USHAURI WA MJOMBA

Mlango uligongwa, Mzee Lemu alikwenda kuufungua, na kukutana na dada yake Ahmad. Walijitoma ndani kimya kimya.

“Karibu! Chukua stuli ukae.” Alikaribisha Mzee Lemu.

“Shikamoo Mjomba.” Alisalimia Mesa.

“Marahaba! Karibu Mpwa’ngu,” Alijibu.

“Kaka! U hali gani?” Mesa alimuuliza Ahmad.

“Sijambo, ninaendelea vizuri,” alijibu Ahmad.

Baada ya salamu, Mesa alibadilisha mada ya mazungumzo na kutumia fursa hiyo ya kukutana kuelezea changamoto inayomkabiri.

***

“Mjomba, wiki iliyopita nilipanga nije. Alhasili, nyumba yangu imetikisika, mume wangu amepata

mwanamke wa nje wenyewe wanaita mchepuko. Sasa mchepuko huo umebadilisha tabia ya mume wangu. Hakipo nitakachokisema kisipate pingamizi wala nitakachokifanya kikakosa kasoro! Kitu kisichokuwa na kasoro ni fedha zangu pekee. Tukiamka, salamu yake ni kuomba fedha. Sasa ninajiuliza, fedha anazoziomba ni za nini? Nilijaribu kumuuliza anakozipeleka, majibu hayakunyooki. Ninavyoona mimi kuwa anapenda fedha zangu kuliko furaha na huzuni yangu," Alianza kulia.

"Watoto mtaniua kwa ugonjwa wa moyo! Haya, ngoja niseme jambo." Mzee Lemu aliwatuliza Wapwa zake kwa sababu huzuri ilirejea tena.  'Mesa mwanangu, tulia! Nitazungumza na mumeo. Lakini vipi bado unampenda? Maana ninyi watoto wakike hamchelewi kusema mume msumbufu kumbe mnatengeneza uzushi katika kuweka mazingira ya kudai talaka ili mtengane.

“Bila kumung’unya maneno, ninampenda sana. Nimeumia nilipojua kuwa ana mwanamke mwingine.”

“Una uhakika ana mchepuko?”

“Ndiyo!”

“Kama ni hivyo, naomba niachie mimi na kila kitu kitakuwa sawa,” alisema kwa kujiamini.

Mesa alimwangalia Mjomba wake kwa moyo wamatumaini.

“Lakini kabla sijakwenda kuzungumza na mumeo, somo linaanza hapa hapa. Wewe binti yangu ni mrembo sana pia msomi mwenye ajira nzuri. Hayupo mwanaume atataka akuache kirahisi na kwenda kuwinda wanawake wengine….!” Mesa alimkata ulimi.

“Malisara ameniacha, yeye sio mwanaume?” Mesa aliona Mzee Lemu yupo upande wa Malisara mwanaume mwenzake.

“Usiwe na hasira mwanangu, sababu haijawahi kujenga. Twende taratibu hadi tutafika kwenye kiini cha tatizo. Jambo la kwanza ninalokuomba, jitathmini na upange upya ratiba yako ya kila siku  kwa sababu inaonekana ina mambo mengi kama ingekuwa kapu lingekuwa limejaa pomoni mwishowe vitu vingine vinashindwa kukaa. Mbaya zaidi aliyeshindwa kukaa kwenye kapu lako ni mwandani wako. Hali hiyo haina afya kwenye ustawi wa familia. Kazi zaofisi na zanyumbani lazima ziendelee na ajira ndiyo inayoboresha maisha ya mtu. Lakini ninaswali la kizushi naoma unijibu kikamilifu.”

“Uliza tu Mjomba.”

“Je, unavyofikiri mumeo nae bado anakupenda au pendo limeshachuja?” Mzee Lemu aliuliza kwa sauti ya upole na mnong’ono.

“Hata sijui. Mimi ninaona ananiomba fedha tu wala hana agenda nyingine yakujadiliana nami,” alijibu Mesa.

“Kwahiyo unadhani anakuomba fedha kwa sababu yeye hana? Kama una mawazo hayo, ujue unakosea. Anakuomba fedha inawezekana hajui anachokitaka. Sababu ni rahisi kupata unachokitaka kuliko kujua unachohitaji, hivyo kujikuta akiomba kilicho rahisi kupatikana. Ukifuata ushauri niliokupa, utaona mambo yote yanakwenda vizuri.”

“Asante mjomba. Nitazingatia ushauri wako,” Alijibu Mesa.

***

Mesa aliporejea nyumbani, alimwalika mume wake kufanya mazungumzo ambayo yalimaliza mgogoro wake na kuishi raha mstarehe.

Kamau alikwenda kwao Mombasa na kubadilisha namba ya simu pamoja na anuani ya makazi. Mara ya mwisho kuwasiliana na Mwantum alimwambia; anasafari ya kwenda Uganda kusalimia ndugu na jamaa. Kutokana na aina ya ajira yake ni ilikuwa ni vigumu kuomba ruhusu isiyo ya lazima kabla ya likizo pia hali yake ya ujauzito inamzuia kusafiri safari ndefu. HivyoMwantum alilea ujauzito akiwa na upweke usiojulikana mwisho wake.

Halikadharika, Ahmad baada ya miezi kadhaa kupita; alifanikiwa kumsahau Mwantum na kujihisi anapata nguvu na ujasiri wakumkabili mwanamke. Mzee Lemu alimwambia Ahmad;

“Jaribu kutafuta mwanamke mwingine, uondoe fikra juu ya Mwantum, sio kweli kuwa wanawake wote ni sawa. Wapo wanawake wengi wenye busara, mapenzi ya kweli na kujiheshimu. Ukimpata wa aina hiyo utasahau machungu yote na kuhisi dunia inazunguka na wewe peke yako. Shukuru Mungu, mmeshindwana mapema. Mwanamke huyu angeweza kupoteza maisha yako kama sio kwa kujinyonga basi ni kwa kunyonga na wewe ukaishia jela ukachinjwe kwa mashine. *‘pancha kabla ya safari ni salama kwasababu ya urahisi wakubadilisha tairi, ingawa itakuchelewesha kuanza safari kuliko bloo ya safarini sababu mara nyingi husababisha kifo au uharibifu mkubwa wa chombo.’’*

MWISHO